**JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUFUNGA MAONESHO YA 46 YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM

**13 JULAI, 2022**
**UWANJA WA MWL. J.K. NYERERE,**
**DAR ES SALAAM**

***Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara;***

***Mheshimiwa Omar Said Shaaban (MBW), Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;***

***Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote mliopo;***

***Mhe, Joketi Mwegelo, DC kny;***

***Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Waheshimiwa Mabalozi, Waheshimiwa Wabunge;***

***Viongozi wote mliopo hapa - Serikali, Dini, Vyama vya Siasi, Taasisi;***

***Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***

***Washiriki wote wa maonesho haya kutoka ndani na nje ya Tanzania;***

***UMAE kutoka Zanzibar; Brassband; Wanahabari;***

***Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana.***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika pamoja siku ya leo, kuhitimisha rasmi Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.

Pia ninakushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Ashatu, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu. Aidha, napongeza Uongozi mzima na watumishi wa Wizara yako; pamoja na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) chini ya Mkurugenzi Mkuu Bi. Latifa Mohamed Khamis; Kamati mbalimbali; Wanahabari; na Wadhamini wote wakiongozwa na Azania Benki waliohusika kufanikisha maonesho haya kuanzia maandalizi hadi mwisho. **Hongera sana! Asanteni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Napenda kuwashukuru wageni waalikwa na washiriki wote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuja kuungana nasi katika Maonesho haya muhimu.

Nimefahamishwa kuwa Maonesho ya mwaka huu yamevutia idadi kubwa ya washiriki kuliko mwaka jana ambapo jumla ya Kampuni **3,200** za Kitanzania na **225** kutoka nchi **23** za Afrika, Asia, Ulaya na Marekani ya Kusini zimeshiriki na waliotembelea maonesho 315,000. Ni faraja kubwa kupata washiriki wengi namna hii, hususan wageni ambapo idadi yao ni takriban mara mbili ya ile iliyofikiwa katika maonesho ya 45. Tunawashukuru sana wote waliotoka nchi za nje na karibuni next maonesho. Hali hii inaashiria kuimarika tena kwa ushirikiano wetu wa kibiashara na mataifa mengine baada ya kuathiriwa na Janga la UVIKO-19. Muitikio wenu mkubwa ndio unaleta maana halisi ya Maonesho haya. Tunawashukuru kwa dhati kabisa. Naomba pia nitoe rai kwenu nyote mlioshiriki au kutembelea mabanda mbalimbali, kuwa huru kutoa maoni na uzoefu mlioupata hapa au kutoka maonesho kama haya katika nchi nyingine ili kutuwezesha sisi kama Serikali kuboresha Maonesho yajayo.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Nimeipenda Kauli mbiu ya maonesho haya inayosema: **"Tanzania; Mahali sahihi pa Biashara na Uwekezaji"** kwa sababu inaakisi vyema nia ya dhati ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuifungua na kuitangaza Tanzania yetu kuwa ni mahali salama kabisa na sahihi pa kufanya biashara na kuwekeza. Ni ukweli ulio wazi Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi, hususan idadi kubwa ya wananchi zaidi ya milioni 60 tena wenye vipaji vingi, ardhi kubwa na nzuri, madini ya kila aina, nafasi ya kipekee ya kijiografia na soko kubwa katika nchi jirani za ukanda wa maziwa makuu. Tanzania ni nchi ambayo amani, umoja na mashirikiano vimetamalaki. Aidha, Serikali imeendelea kujenga mazingira rafiki ya Uwekezaji na Biashara ili kuvutia uwekezaji. Kwa mfano katika hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali 2022/23 Serikali ilitangaza hatua mbalimbali za kikodi na kiutawala kwa lengo la kuzidi kuyafanya mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza kuwa rafiki zaidi. Hatua hizo ni pamoja na kutoa nafuu za kikodi kwa wazalishaji na wafanyabiashara; kuendelea kufuta kodi na tozo za kero; kuongeza bajeti ya Kilimo ili kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mali ghafi viwandani; kuweka utaratibu wa hati miliki ili kulinda haki za wasanii na kuchochea upatikanaji wa ajira kwa vijana. Hatua nyingine ni kuweka msukumo katika kuboresha miundombinu ya umeme ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati kupitia Gridi ya Taifa; kupanua na kujengea uwezo Bandari zetu, hasa Dar es Salaam, ili kuongeza ufanisi; na kuendelea kuimarisha Shirika la Ndege ili kuwa na usafiri wa anga wa uhakika zaidi.

Vilevile, kupitia ziara za Mheshimiwa Rais katika nchi mbalimbali na filamu yake ya "Royal Tour" tumeanza kushuhudia wawekezaji mbalimbali kuja

kuwekeza katika Sekta mbalimbali nchini na watalii wengi zaidi kutembelea nchi yetu. Nawasihi watanzania kwa ujumla, na hasa Sekta Binafsi, kujipanga na kuwa tayari kuchangamkia fursa hizo zinazoibukia kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Maonesho haya yanathibitisha kuwa watanzania wanashauku kubwa ya kufanya biashara, kuweka na kufanya kazi kwa bidii kuendeleza nchi yao na familia zao. Aidha, maonesho haya ni fursa ya kuonesha na kutangaza bidhaa mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini. Mikataba iliyosainiwa ($76m); SINOTAC ($171m) Certificate of incention. Haya ni mafanikio makubwa sana. Yanafurahisha. Si hivyo tu, kupitia maonesho haya, wananchi wamepata fursa ya kujifunza namna tunavyoweza kukuza biashara na nchi nyingine. Elimu: fursa za mikopo, virutubisho, vyakula mbalimbali. Watanzania wengi wanajituma lakini ili wanufaike na faida zinazotokana na nchi yetu kuwa mwanachama wa soko kubwa la EAC, SADC na AfCFTA (Eneo Huru la Biashara Afrika) ni lazima kujipanga na kushirikiana sisi kwa sisi lakini pia na wadau wengine. Tunaweza kujipanga vizuri kwa makampuni na wazalishaji hapa nchini kushirikiana na hata kuwawezesha kushindana eg Kampuni inayounganisha magari; kuingia ubia; kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya usafiri; usafirishaji; mawasiliano; na maghala ili kuunganisha watu na masoko, kuweka nguvu katika upatikanaji wa teknolojia bora na kuondoa vikwazo visivyo vya lazima kwa biashara na uwekezaji. Serikali kwa upande wake imeendelea kushughulikia changamoto hizi ili kutoa nafasi kwa wafanyabiashara na wawekezaji kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo na zinazochipukia. Ni muhimu pia kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi na kupeana majukumu ya kutanzua changamoto mbalimbali za kibiashara ili wananchi wetu waweze kunufaika zaidi na zaidi.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Kama wote tunavyokumbuka biashara nyingi, hasa ndogo na za kati, zilianguka au kurudi nyuma sana kutokana na janga la UVIKO-19. Mitaji ilianguka, madeni yakawa hayalipiki na wateja nao walipungua, gharama za kupanga maeneo ya biashara zikawa mzigo, baadhi ya biashara zilifungwa na watu wakapoteza ajira. Bahati nzuri, hivi sasa Sekta ya Biashara na Viwanda nchini, inaendelea kuimarika baada ya janga la UVIKO-19. Shughuli za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo bidhaa za chuma, saruji, vigae, nguo na mavazi, ngozi na bidhaa zake, nyama za kusindika, chakula, mbogamboga na matunda zimeongezeka, hali ambayo imechochea pia ajira

kuongezeka kufikia 370,485 (2021) ukilinganisha na ajira 336,797 mwaka 2020.

Fundisho muhimu kutokana na janga la UVIKO-19 ni kwamba, wafanyabiashara na wajisiriamali wetu ni lazima watafakari upya namna ya kuendesha biashara zao, kuziimarisha na kuwa wabunifu zaidi ili kuweza kuendana na changamoto za kiuchumi zinazotokana na majanga mbalimbali kama magonjwa ya mlipuko au moto. Ujasiri na kutokata tamaa ndio siri ya mafanikio katika biashara/ujasiriamali. Kwa mfano, kufuatia changamoto ya UVIKO-19 baadhi ya wafanyabiashara walianza kufanya biashara kwa kutumia mitandao. Hali kadhalika, baadhi ya watanzania walianza kununua bidhaa kupitia mitandao na kufanya miamala kielektroniki. Makampuni ya mawasiliano nayo yalianza kutengeneza programu kuwezesha wajasiriamali kufanya biashara, kupata mitaji na kufikia masoko kupitia njia za kidijitali. Nawapongeza hao wote kwa kuwa wabunifu na kuendelea kuwahudumia watanzania.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Na mimi nimepata fursa ya kutembelea baadhi ya mabanda na kuzungumza na washiriki na wananchi waliokuja kutembelea maonesho haya. Nimefurahi na ninawapongeza tena waandaaji ninaposhuhudia kwamba, tofauti na mwaka jana, zamu hii mmetenga maeneo maalum ya kisekta ikiwemo Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Madini, Wajasiriamali wadogo kupitia SIDO, Wamachinga pamoja na Wasanii. Lakini pia ushiriki wa Taasisi za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na Taasisi za Utafiti, Bunifu, Vyuo Vikuu na huduma za kijamii umeongezeka. **Hongereni Sana!** Nimeona mambo mengi mazuri na changamoto na bila shaka Wizara na TanTrade nanyi pia mmepokea ushauri na maoni ambayo naamini mtakwenda kuyafanyia kazi.

- Masoko
- Upatikanaji wa vifungashio vyenye ubora
- Elimu ya biashara na vyanzo vya mitaji
- Malighafi za batiki, cooking oil
- Tekinolojia za uongezaji thamani
- Masharti ya taasisi za urekebishaji na ubora wa viwango
- Changamoto za kisheria

Utafiti

- Mbegu za mafuta
- Kubuni mashine za agro proc

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Napenda kuhitimisha hotuba hii **kwanza** kusisitiza wito wangu niliotoa katika

maonesho ya mwaka jana kwa wazalishaji wetu nchini kwamba mzingatie kanuni za ushindani katika soko, ikiwemo kuheshimu mikataba na kuzalisha bidhaa bora na za viwango vya juu. Aidha, ongezeni uzalishaji wa bidhaa ambazo zina mahitaji makubwa nchini kama sukari, mafuta ya kupikia, unga wa ngano na bidhaa za ujenzi ikiwemo mabati, nondo na saruji. Naamini tukidhamiria, tunao uwezo wa kujitosheleza kwa matumizi ya ndani na kuwa na ziada ya kuuza nje ya Nchi. Aidha, nawasihi Watanzania wenzangu, tupende na kujivunia vya kwetu. Tuunge mkono wajasiriamali wetu kwa kununua zaidi bidhaa zetu za ndani ili kutengeneza ajira, kukuza pato la mtu binafsi na Taifa kwa ujumla. Nawaomba pia, wajasiriamali kuchangamkia fursa za mafunzo zinazotolewa na Taasisi mbalimbali za ndani na za Kimataifa (kama SIDO, mabenki, Vyuo vya Elimu ya biashara, UNIDO n.k.).

**Jambo la pili**, kama mnavyofahamu, Tanzania ni moja ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Umoja wa Afrika (AU). Pamoja na kuondolewa kwa ushuru wa forodha na kuweka vivutio mbalimbali ilikuongeza zaidi uwezo wetu wa kuzalisha bidhaa za nafaka, nyama, samaki, matunda na mbogamboga, bado kiwango cha biashara yetu katika masoko haya ya kikanda iko chini ya asilimia 20! Hivyo napenda niwasihi Watanzania, tutumie fursa hizi katika kuongeza wigo wa masoko ya bidhaa zetu, ikiwemo kujipanga kikamilifu kuuza katika eneo huru la kibiashara la Afrika (AfCTA) lenye takriban watu bilioni 1.3. Na hapa nawaelekeza TanTrade na Wizara zetu (SMT na SMZ): toeni elimu zaidi ya masoko haya kwa wafanyabiashara wetu ili waweze kuchangamkia na kunufaika na fursa hizi.

**Jambo la tatu,** ninaitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya jitihada za makusudi kubaini vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha vinavyokwamisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za Bara la Afrika hasa nchi wanachama wa EAC na SADC, visivyoendana na sheria na makubaliano yetu. Aidha, Wizara ishirikiane na wafanyabiashara pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Rais kwa Taasisi zote za Umma kurahisisha mazingira ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji hapa nchini. Fuatilieni kwa karibu kuona kama kweli urasimu, ikiwemo katika upatikanaji wa vibali mbalimbali vya biashara /uwekezaji nchini, unaondolewa kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (*Blue Print*). Wafanyabiashara nawaomba mtoe taarifa kuhusu changamoto ambazo bado mnakumbana nazo huko TRA, TBS, BRELA, TMDA na Idara nyingine za Serikali ili tuzivalie njuga!

**Jambo la Nne,** Wizara ya Viwanda na Biashara (SMT na SMZ) na TanTrade

shirikianeni na Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, mboreshe Kanzidata ya taarifa za biashara na fursa za masoko kwa kuhakikisha ni toshelevu na zinapatikana kwa wakati (*real time*). Nimetembelea Tovuti zenu na kubaini kuwa taarifa za masoko hazijanyumbuishwa kwa ufasaha kumsaidia mzalishaji au mfanyabiashara, au mwekezaji kuzitumia.

**Jambo la Tano**, ninatoa rai kwa wafanyabiashara na makampuni ya mawasiliano, TRA na BRELA muwekeze, kwa nguvu na kasi Zaidi, katika teknolojia za kidigitali ikiwa pamoja na kutambua na kurasimisha biashara mbalimbali zinazofanyika kidijitali. Aidha, wajitahidi kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wafanyabishara na wawekezaji kwa njia ya kidigitali.

**Jambo la Sita,** ninakiri kuwa Sekta ya fedha (BoT, Benki za Biashara na Taasisi mbalimbali za fedha) zimefanya jitihada za kuridhisha katika kubuni madirisha ya mikopo, mitaji na mafunzo kwa wafanyabiashara na wajasiriamali. Ninachowaomba watanzania, ni kwamba tuchangamkie fursa hizo. Na kwa upande wa Benki nao ninawataka mwendelee kuboresha zaidi huduma hizo ili wajasiriamali zaidi wapate mitaji ya kuanzia biashara (start-up capital). Katika hili bado changamoto ni kubwa.

**Mwisho,** mwaka jana katika uwanja huu huu niliwashauri TanTrade mfikirie kuwa na utaratibu wa kujiwekea malengo ya maonesho haya ya Biashara ya Kimataifa na kujipima mmefanikiwa au mmeshindwa kiasi gani, na hata kujilinganisha na maonesho mengine ya Kimataifa. Aidha, nilipendekeza mkusanye maoni na ushauri wa washiriki wa maonesho na wadau ili kuboresha zaidi maonesho yanayofuata. Lakini nimetembelea *Tovuti yenu ya TanTrade nikakuta eneo la Mpango Mkakati na Ripoti ya Mwaka vikiwa tupu! Pia katika eneo la machapisho sijaona* ***Kitabu kuhusu Tathmini ya Maonesho*** *yaliyopita*. Ninatoa tena rai mlitafakari hili. Mimi bado naamini ni jambo zuri la kufanyia kazi.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Kuhitimishwa kwa Maonesho haya ya 46 ni mwanzo wa maandalizi ya Maonesho ya 47. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kuwatakia nyote kila la kheri na safari njema muendako. Vilevile, Serikali inawaalika Wadau wote kushiriki kwenye ***Maonesho ya Saba (7) ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania*** yatakayofanyika katika uwanja huu huu sambamba na maadhimisho ya sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara kuanza tarehe **05 – 09 Desemba, 2022** yakilenga kutangaza fursa za bidhaa za viwanda zinazozalishwa hapa nchini.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Mwisho kabisa, napenda kuwakumbusha wafanyabiashara, wenye viwanda na wananchi wote kuhusu utunzaji wa mazingira. Tuitunze na kuilinda ekolojia ya nchi yetu nzuri kwa kutunza misitu, kupanda miti na kufanya usafi wa mazingira ya biashara zetu na maeneo ya uzalishaji viwandani wakati wote. Aidha, naomba kuwakumbusha pia watanzania wote kuwa tarehe 23 Agosti 2022 ni siku ya Sensa ya Watu na Makazi. Nawaomba wananchi wote wajitokeze kuhesabiwa na kutoa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

Baada ya kusema haya, naomba sasa kutamka rasmi kuwa: **Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwa mwaka 2022, sasa yamefungwa rasmi.**

**Mungu Ibariki Tanzania,**
**Asanteni kwa kunisikiliza!**